

PEPONI NDIO MAKAZI

1. Ninaingia kwa dhati, imani kuitangaza
Katika zote nyakati, dini hutupa mwangaza
Tusifanye tashtiti, na Ibada kupuuza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
2. Ibada ndio tiketi, peponi kutuingiza
Tukamilishe swalati, mitume waloagiza
Na swaumu na zakati, shahada tukitimiza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
3. Kuhiji ni jambo nyeti, Kwa kila anayeweza
Kwa kila mwenye manoti, ni bora kujihimiza
Ukapande Arafati, na mola kumtukiza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
4. Ninaipaza sauti, wenzangu kuwahimiza,
Yasijefika mauti, yakukute unabweza
Ya akhera akaunti, toba hujatanguliza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
5. Jenga nyumba madhubuti, ya imani kukomaza,
Usijenge ya makuti, Shetani ataunguza,
Ni bora uwe smati, wasije wakakukwaza,
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
6. Utajafika wakati, Mauti kujitokeza,
Yatakuja kama nyati, wala hayataki viza,
Nuru tena huipati, macho yatajaa kiza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
7. Hazitakufaa suti, ukishapanda jeneza,
Utasikiza sauti, kuzijibu hutaweza
Umeshafika wakati, dongo kukukandamiza,
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
8. Na wala hufurukuti, kaburi likikumeza
Roho tena huipati, Izraili kaipaza
Hadi saba samawati, kwenye kumbi la gereza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
9. Uwapo ulisaliti, Na wenzio kuwaponza,
Na kufanya harakati, watu ukawachukiza
Utaionja baruti, na moto wa kuunguza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
10. Kule hakuna kamati, ya kuja kukuliwaza,
Wataka mwenzi hupati, ila majoka na funza
Raha hapo hazipiti, madhambi huzifukuza.
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
11. Kamwe haufurukuti, mauti yakikumeza,
Haya si nusu kaputi, uhai kuurejeza,
Ajali ikithibiti, siku hiyo hutacheza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
12. Mbele ya mola uketi, hukumu ukisikiza,
Iwapo ulishatiti, na watu kuwapoteza,
Msamaha haupati, hata uote kengeza,
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza
13. Thilitashara beti, yanibidi kutuliza,
Ni wajibu kusukuti, baada ya kueleza,
Iendee misikiti, na mema kutekeleza
Peponi ndio makazi, kutubu nawahimiza

Said bin Sultan

Box 256 pc 119

Oman.

Said_almughairy@hotmail.com